

Bibilia ya watoto

Inaleta

Agano ya
Mungu kwa
Ibrahimu




Kimeandikwa na: Edward Hughes
Kimeorodheshwa na: Byron Unger; Lazarus
Alastair Paterson
Imerekebishwa na: M. Maillot; Tammy S.
Kimetafsiriwa na: Grace Chepkoech
Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org

BFC
PO Box 3
Winnipeg, MB R3C 2G1
Canada

©2022 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.





Kitambo baada ya mafuriko,
watu duniani walipanga mpango.
"Tutajenga mji na kilele chake
kifike mbinguni," wakasema
"Halafu tuishi sote pamoja kila
siku." Wote walizungumza
lugha moja.




Mungu aliwataka watu waishi kote duniani alimoumba.
Sasa, akatenda jambo la kipekee.
Mara tu, vikundi tofauti wakaanza
kuzungumza lugha tofauti. Mungu
aliwapa lugha mpya.



Wale ambao walizungumza lugha sawa wakaenenda pamoja. Kwa sababu ya haya watu wakaanza kuogopana. Katika jinsi hii, Mungu akaweza kufanya watu kuishi katika nchi tofauti. Mji ule ambao walikuwa


wameanza




kujenga
uliitwa Babeli,
inayomaanisha
kuchanganyikiwa.




Miaka ilipopita,
mahali palipoitwa
Uru wa Wakaldayo,
Mungu alizungumza
na mtu aliyeitwa
Abramu. "Toka
nchini mwako,"
Mungu akaamuru.
"Nenda nchini
nitakapow-
aonyesha."




Abramu akatii. Mungu alimwongoza hadi Kanaani. Mkewe Sarai na mwana wa nduguye Lutu wakaenda naye pia.



Kule Kanaani Abram na Lutu wakawa
tajiri. Walikuwa na mifugo lakini
hakukuwa na malisho ya kutosha
kwa wanyama wengi vile.




Wachungaji wa Lutu wakawa na
ugomvi na wachungaji wa Abramamu.
"Basi, kusiwepo ugomvi," Abramamu
akasema. "Tutatengana. Lutu,
chagua unapotaka."




Lutu akachagua nchi yenye nyasi tele
ikiwa na miji na vijiji. Kulionekana
kuzuri lakini miji ile ilijaa maovu.



Baada ya Lutu kuondoka, Mungu alizungumza tena na Abramamu. "Nitawapa mji wa Kanaani wewe na watoto wako milele." Abramamu na Sarai hawakuwa na watoto. Mungu angetimiza aje agano yake?





Watu
watatu
kutoka
kwa Mungu
wakawajia

Abramu na Sarai.

"Mtaweza kupata mtoto hivi karibuni," wakasema. Sarai alicheka sana. Hakuamini neno la Mungu. Yeye alikuwa wa miaka tisini. Mungu akamwambia Abram kuwa ataitwa Ibrahimu na Sarai ataitwa Sara.







Mungu pia akamwambia Ibrahimu kuwa angeangamiza miji miwili yenye uovu ya Sodoma na Gomora. Mwana wa nduguye Ibrahimu, Lutu aliishi Sodoma pamoja na familia yake.



Lutu aliamini hadhari
ya Mungu ilipokuja,
lakini mabwana wa
binti zake walikataa
kutoka Sodoma.
Ilikuwa mbaya aje!
Hawakuamini neno
la Mungu.




Lutu na Binti wake ndio walioponea.
Kiberiti na moto ikanyesha katika
miji ile yenye maovu.



Kwa bahati mbaya mkewe Lutu
akakosa kumtii Mungu na akatazama
nyuma alipokuwa akitoroka.
Akabadilika na kuwa
nguzo la chumvi.



Mungu
akatimiza ahadi
yake kwa
Ibrahimu na
Sara. Walizaa
mtoto katika
uzee wao, jinsi
Mungu alikuwa
amesema.
Walisherehekea
sana Isaka
alipozaliwa!



Pengine Ibrahimu pia
alifikiria kuhusu agano ya
Mungu ya kuwapa yeye na
watoto wake mji wa
Kanaani milele. Mungu
angetimiza ahadi ile
pia. Mungu hutimiza
ahadi zake.



Agano ya Mungu kwa Ibrahimu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Mwanzo 11-21

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."

Zaburi 119:130





Mwisho



4



60



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

